# MAISHA YA MTUME
# MUHAMMAD
# s.a.w.





Kimeenezwa na
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
S.L.P. 376 Dar es Salaam
Tanzania

**MAISHA YA MTUME MUHAMMAD S.A.W.**

**Mtunzi:** Al-Haj Maulana F. R. Hakeem
**Mfasiri:** Maulan Sheikh Mubarak Ahmad

© Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

Chapa ya mara ya kwanza - 1956

Chapa ya mara ya tisa - 1994
(Nakala 30,000)
Chapa ya Mara ya kumi - 2005
Nakala 2,000
2005

**ISBN 9987 - 438 - 01-6**

Kimeenezwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
S.L.P 376
Simu 2110473 . Fax 2121744
Dar es Salaam

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema na Ukarimu**

## UKUMBUSHO

Kitabu hiki kinachotangazwa juu ya “Maisha ya Mtume Muhammad (SA W)” katika lugha ya Kiswahili ni tafsiri ya kile kitabu kilichotungwa na Al-Haj Maulana F.R. Hakeem kwa Kiingereza kiitwacho “The Life of Muhammad” ambacho kilienea sana katika bara la Afrika toka magharibi mpaka mashariki.

Mtungaji wa kitabu hiki Maulana Hakeem alikuwa Mwanachuoni maarufu na mbashiri mtawa wa Kiislam kwa muda wa miaka ishirini katika nchi mbalimbali za Afrika ya Magharibi. Katika siku za kukaa kwake huko alipokuwa akishughulika katika kazi ya kueneza dini ya Kiislam yeye alikuwa msimamizi wa shule nyingi za Kiislam pia. Katika maendeleo ya kazi hiyo aliona kwa sikitiko kubwa kuwa watoto wanafunzi, hata watu wazima, wengi katika Waislamu, hawajui hali ya maisha ya Mtume Muhammad (SA W) ambaye ndiye Nabii kamili kwa watu wote. Hivyo akapata wazo la kutunga habari za maisha matakatifu ya Mtume Muhammad (SAW) pamoja na kazi yake tukufu na sifa zake njema kwa kifupi ili watoto na wanafunzi wa shuleni na wengine wasio na maarifa waelewe kidogo jinsi ilivyokuwa hali ya mwanzilishi mtakatifu wa Uislam.

Tumeiona hali hiyohiyo katika sehemu hizi za Afrika Mashariki. Watoto kwa wakubwa - wengi zaidi katika hao - toka Ujiji mpaka Entebbe na toka Bukoba mpaka Mtwara hawana maarifa ya kutosha ya hali na maisha ya Mtume Muhammad (SAW). Hivyo ilitakiwa kutangaza vitabu vingi tena kwa maelfu ili Waislamu na wasio Waislamu wapate kujua hali ya kweli ya maisha ya Mtume Muhammad (SAW). Kwa wakati wa sasa tumekikuta kitabu hiki kidogo ni kizuri mno kwa makusudio yetu na tunatangaza tafsiri yake kwa Kiswahili neno kwa neno, bila kupunguza au kuzidisha lolote ndani yake, kwa lugha nyepesi ili wenyeji wasiwe na taabu ya kukifahamu.

Mtungaji maarufu wa kitabu hiki alifariki mwaka jana baada ya kurudi kwake huko Pakistan. Twaona kuwa kutangazwa kwa kitabu hiki kwa Kiswahili ni ukumbusho mzuri wa marehemu Maulana Hakeem na kazi yake yenye thamani sana aliyoifanya kwa kuitukuza dini ya Islam.

Twamwombea raha na amani na mahali pema milele na milele. Amin.


**Sheikh Mubarak Ahmad,**
1956 A.D.

Mbashiri wa kwanza kuletwa Afrika ya Mashariki.

# YALIYOMO

**SURA YA KWANZA:**
Kuzaliwa kwake na ukoo wake - uchanga wa Muhammad - utoto wa Mtume Muhammad (S.A.W.) ... ... ... ... ... ... 1
**SURA YA PILI:**
Umbo lake - uthabiti wake - utukufu wake - imani na haki yake - Al-Amin ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 5
**SURA YA TATU:**
Ndoa yake na bi Khadija - aliwafanya huru watumwa- maisha yake ya ibada ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 8
**SURA YA NNE:**
Kuitwa kwake - Abu Bakr kwenda pamoja naye – mateso kwa imani yao - njia yake ya kueneza ujumbe wake - mateso zaidi kwa wafuasi wake ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 11
**SURA YA TANO:**
Mafunzo ya Mtume - itikadi za watu wa nchi yake - kazi yake ya ajabu - itikadi katika ushirikina - hali ya wanawake . ... ... ... .... ... ... ... ... ... 17
**SURA YA SITA:**
Wasio na makao waliohitaji msaada kwenda Uhabeshi nyakati mbaya katika Makka . ... ... ... ... ... ... ... ... 21
**SURA YA SABA:**
Safari ya kwenda Taif - kuenea kwa Uislam Madina- kukimbilia Madina ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 26
**SURA YA NANE:**
Mtume kuchaguliwa mfalme wa Madina - vita vya Mtume kisa cha Uhud ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 32
**SURA YA TISA:**
Kisa cha Hunain na nguvu za Utume - hotuba ya mwisho ya Mtume ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 37
**SURA YA KUMI:**
Tabia ya Mtume - Mafundisho ya Mtume ... ... ... ... ... 42

## RAMANI YA BARA ARABU



## SURA YA KWANZA

### Kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W) na Ukoo wake

Kama miaka elfu moja na mia nne iliyopita, siku ya tarehe 20 Aprili 571 A.D., mtoto alizaliwa Makka, mji katika Bara Arabu kiasi cha maili arobaini kutoka kwenye ukingo wa bahari ya Red Sea (Bahari ya Shamu). Mtoto huyo alikuwa Mtume mtakatifu Muhammad (S.A.W).

Jina aliloitwa mama yake mtoto huyo ni Bi Aaminah, binti wa Wahab bin Abdu-Manaf, ambaye alikuwa wa ukoo wa Zuhra, Baba yake naye aliitwa Abdullah, wa ukoo wa Banu Hashim.

Baada ya siku kidogo Abdullah kumwoa Bi Aaminah, Abdullah alikwenda Shamu (Syria) katika msafara wa biashara. Alipokuwa akirejea nyumbani alishikwa na maradhi na akafa katika Madina; wakati huo mji huu ulijulikana kwa jina la Yathrib. Kwa hivyo Muhammad (S.A.W) alizaliwa akiwa yatima asiye na baba.

Kabla ya kuzaliwa Mtume mtakatifu (S.A.W), mama yake aliota kuwa kesha mzaa. Pia aliota kuwa lazima aitwe Muhammad maana yake asifiwaye. Aaminah aliona katika ndoto nyingine nuru kubwa inatoka katika mwili wake na kutapakaa katika nchi zote.

### Uchanga wa Muhammad (S.A.W)

Watu wa Makka walikuwa wakiwapeleka watoto wao wachanga kwenda kulelewa na wanawake wa vijijini ambako hewa za huko zilikuwa nzuri zaidi kuliko hewa ya mjini.

Wanawake wa vitongoji kiasi cha maili thelathini au arobaini kutoka Maka walizoea kuja mjini na kuwachukua watoto wachanga waliozaliwa na kwenda nao kuwalea.

Wanawake hawa walilipwa ujira wa kuwalea hawa watoto na wazazi wa watoto walipowarudisha wakati wa malezi ulipokwisha.

Bi Aaminah alitaka mmoja wa mayaya hao kumlea Mtume Muhammad (S.A.W). Kila mmoja miongoni mwa wanawake hao aliposikia kuwa baba wa mtoto huyo amekufa alikataa kumlea, kwa kuogopa kuwa hatalipwa pesa za kutosha. Hawakujua kuwa yeye ndiye atakayekuwa Bwana wa Wafalme na Watawala.

Njia za Mungu ni kinyume na njia zetu. Mungu Alikwisha panga jinsi Aaminah atakavyopata furaha na kuridhika, na jinsi Mtume Muhammad (S.A.W) atakavyolelewa kijijini.

Miongoni mwa hao waliokuja Makka kuchukua watoto alikuwako mwanamke mmoja masikini, jina lake Halimah. Alibisha nyumba baada ya nyumba, akiuliza mtoto wa kulea lakini hapana wazazi waliotaka kumkabidhi mtoto wao kwa mwanamke masikini.

Baada ya kukosa kumpata mtoto katika nyumba nyinginezo zote alikata shauri kumchukua huyo mtoto aliyekuwa hana baba, ili wanawake wengine wasije wakamchekelea kurejea nyumbani pasipo na mtoto aliyemchukua.

## Utoto wa Muhammad (S.A.W).

Muhammad (S.A.W) alipotimu miaka minne, Bi Halimah alimrejesha kwa mama yake, ambaye baada ya miaka miwili mingine alimpeleka kwa wazee wake katika mji wa Madina. Baada ya kukaa Madina kwa mwezi mmoja, walipokuwa wakirejea Makka pamoja na mtoto, Bi Aaminah alikufa wakiwa safarini. Kwa hiyo katika umri wa miaka sita Mtume Muhammad (S.A.W) aliachwa yatima asiye na baba wala mama. Mtu mmoja alimchukua na kumpeleka kwa babu yake Makka Bwana Abdul Mutwalib, lakini baada ya miaka miwili babu huyu naye alikufa, na hivyo Mtume Muhammad (S.A.W), akiwa na umri wa miaka minane alikwenda kuishi na baba yake mdogo aliyeitwa Abu Talib.

Nyumba Mtume Muhammad (S.A.W) alimoishi alipokuwa mtoto hazikuwa za kitajiri, na watoto wengine hawakuwa na adabu nzuri. Wakati wa chakula ulipofika watoto walimzunguka mama yao, na kuitisha kwa sauti za juu kila chakula walichotaka. Kila mmoja alijaribu kupata chakula kingi kuliko wenzake. Lakini walipopiga kelele, Mtume Muhammad (S.A.W) alijikalia peke yake na kunyamaa, akimngoja mama yake mdogo (mke wa Bwana Abu Talib) ampe chakula, na alikula kwa furaha chakula cho chote alichopewa.

Hata katika wakati huo wa umri mdogo, kila mtu aliyemjua Mtume Muhammad (S.A.W) aliona matendo yake yenye fikira; na baba yake mdogo alimpenda sana hata alitaka Mtume Muhammad (S.A.W) awe naye wakati wote, mchana na usiku.

Katika siku hizo walikuwa watu wachache katika bara Arabu walioweza kusoma ama kuandika, na kwa hivyo Mtume (S.A.W) alikuwa pasipo kujua mafunzo yoyote ya vitabu. Watu

walistaajabu kuwa Mtume Muhammad (S.A.W) alijua mambo mengi na alikuwa mtu mwenye busara sana ingawa hakuwa na ujuzi wa kusoma.

Mtume Muhammad (S.A.W) alipokuwa na miaka kumi na miwili, baba yake mdogo alikuwa lazima aende Shamu kwa msafara wa biashara. Kijana huyu hakuweza - kustahimili upweke wa kumkosa baba yake mdogo kwa kutengana nae kwa muda mrefu hiyyo. Kwahiyo Abu Talib alimchukua Mtume Muhammad (S.A.W) pamoja nae safarini. Njiani walionana na mtu wa dini, Mkristo aliyeitwa Bahira, aliyeuona uso wa Mtume (S.A.W) na kuona alama za umaarufu wake wa siku zijazo. “Mtunze mwana huyu”. Bahira alimwambia Abu Talibu. “kwa sababu siku moja atapata kazi ya kumtumikia Mungu.

## SURA YA PILI

### Umbo lake

Mtume Muhammad (S.A.W) alikuwa na uso wa kawaida, lakini hata hivyo ulimwonyesha kuwa mtu wa maana sana. Mwili na urefu wake ulikuwa wa kadiri ya katikati, yaani si mrefu sana wala si mnene sana; alikuwa na kichwa kikubwa kilichoumbika vizuri, na kipaji kipana. Macho yake meusi yalionekana yamejaa nuru na yalikuwa na kope ndefu. Meno yake yalikuwa meupe sana. Nywele zake nyeusi zilikuwa kubwakubwa. Rangi ya ngozi yake ilikuwa ile nyeupe-nyekundu. Sura yake na adabu zake zilikuwa za kupendeza sana hata ikawa alivuta nyoyo za watu wote waliomwona.

Ingawa Mtume Muhammad (S.A.W) wakati mwingine alicheka, kwa kawaida alikuwa mnyamavu mwenye fikira nyingi na kwenye midomo yake kwa kawaida alikuwa na tabasamu kubwa la kupendeza. Moyo wake ulikuwa thabiti sana, alikuwa na fahamu ya upesi, na uwezo wake mkubwa wa kukumbuka mambo, na akili nyingi ya kuwazia mambo. Mazungumzo yake kwa kawaida yalikuwa ya upole lakini thabiti, sauti yake ilikuwa nzuri na yenye nguvu. Hakupata kuvaa nguo ghali, kwa sababu alifikiri kuwa ni ujinga kujisumbua kwa mambo ya namna hiyo.

### Uthabiti wake

Tangu utoto wake tabia yake ilikuwa ni safi na thabiti. Abu Talib alimwambia Abbasi ndugu mdogo zaidi wa baba yake Mtume Muhammad (S.A.W) sijapata kumsikia Muhammad akisema uwongo wala kumwona akicheza na watoto barabarani. Mtoto huyu ni wazi hakupenda kule kugombana na kupigana ambavyo vilikuwa ni sehemu ya michezo hii ya barabarani.

Katika siku hizo watu wa Bara Arabu walikuwa na itikadi nyingi za kijinga, na waliabudu masanamu badala ya Mungu. Lakini hakukuwa na jambo alilolichukia Mtume Muhammad (S.A.W) sana kuliko kuabudu sanamu. Hata tangu siku zake za utoto hakupata kutenda jambo hili hata siku moja, na kila wakati alikataa kula chakula chochote kilichohusiana na sadaka zilizotolewa kwa masanamu.

## Utukufu wake

Wazee husema "Vijana wana wazimu, vijana hawawezi kuona yaliyo haki." na mara nyingi haya huwa kweli. Tunapokuwa vijana huficha sheria za dini na tabia za haki, na wengi kati yetu hufikiria starehe tu. Lakini tunapoanza kuwa wazee twatambua matendo yetu mabaya na mambo ambayo tumeyakosa. Hapo baadhi ya watu huenda kuishi katika misikiti au katika majumba wanamoishi watawa, ambako huishi ili kufanya ibada kuwa kazi yao ya siku za uzee. Lakini hata maisha ya awali ya mtukufu Mtume Muhammad (S.A.W) yalikuwa si ya kulaumiwa, na ni lazima kuinamisha vichwa vyetu kwa heshima tunaposoma juu yake.

Katika Bara Arabu, miaka elfu moja na mia nne iliyopita, Mtume Muhammad (S.A.W) alipokuwa mtoto, watu walikunywa vinywaji vikali, wanaume waliishi na wake wa wanaume wengine, wanawake waliuza miili yao wenyewe kwa wanaume, hata wasichana walikuwa hawana salama miongoni mwa wanaume. Waarabu hata hivyo walikuwa wakiona fahari juu ya mambo yao maovu na maisha matakatifu ya Mtume Muhammad (S.A.W) katika watu kama hawa ni moja katika mambo yaliyo miujiza mikubwa ya Dunia. Matendo yake ya kila siku katika siku hizo za awali za maisha yake Mtume Muhammad (S.A.W) yanajulikana vizuri kama yale ya siku za baada ya kupata utume, na hata maadui zake wabaya kabisa hawajaweza kuthubutu kupinga ukweli kwamba maisha yake ya utoto na ujana yalikuwa mazuri na safi.

Alijitenga na watu wote wabaya na alikuwa na marafiki wachache sana, lakini marafiki hawa aliokuwa nao walifuata mafundisho yake na mwishowe wakasilimu. Ingawa vijana wenzake wa rika lake walipitisha wakati wao katika maisha mabaya, Mtume Muhammad (S.A.W) alikuwa akitafuta njia ya kuokoa Bara Arabu kutokana na hali yakusikitisha ambayo nchi hii ilikuwa imeingia. Kurani Tukufu inaeleza utukufu wa tabia yake katika aya ya (10:17) ambayo maana yake ni "Nimeishi wakati mrefu na ninyi, na mwajua vizuri sana kwamba sijapata kusema uwongo hata juu ya mtu. Vipi sasa nitawezaje kusema uwongo juu ya Mungu. Kwa nini hamwamini mafundisho yangu?"

**Imani na haki yake**

Mapenzi ya Mtume (S.A.W) kwa masikini, watu ambao hawawezi kujisaidia, mayatima na wanawake waliofiwa na waume zao, yalikuwa ni makubwa sana. Alifanya kama uwezo wake ulivyomwezesha kuwasaidia. Hata alipokuwa na umri wa miaka ishirini tu, alikuwa mwanachama wa chama cha kulinda wanyonge. Wanachama wote wa chama hiki waliahidi kwamba watamsaidia na kumhami mtu yeyote ambaye alifanyiwa vibaya, yeyote awaye. Kwahivyo tangu siku zake za ujana Mtume Muhammad (S.A.W) alimpa msaada yeyote Aliyeuhitaji, na hakuweza kutulia mpaka haki iwe imefanywa.

**'Al-Amin'**

Katika wakati huu uaminifu wa Mtume (S.A.W), Ukweli, imani na utukufu vilimfanya kupewa jina la Heshima la Al-Amin, neno la kiarabu ambalo lina maana mbili yaani 'mwaminifu mkweli'na pia 'mwenye kuaminiwa'. "Al-Amin' maana yake si uaminifu kwa mambo yahusuyo pesa tu, bali kwa kila kitu. Watu ambao siku hizo walikuwa na uhusiano wowote na Mtume Muhammad (S.A.W) kila mara walisema maneno ya sifa Kumhusu yeye.

## SURA YA TATU

### Ndoa yake na Bi Khadija

Sifa ya utukufu na uaminifu wa maisha ya Mtume Muhammad (S.A.W) vilipoenea sehemu zote za nchi, aliandikwa kazi na bibi tajiri mfanya biashara wa Makka, ambaye jina lake lilikuwa Khadija. Kazi hiyo ya Mtume Muhammad (S.A.W) ilikuwa ni kufanya msafara wa biashara kwenda Shamu. Aliahidiwa kupewa sehemu ya faida ya biashara hiyo yake. Bi Khadija alimpa mmoja wa watumwa wake aandamane naye safarini. Mtume Muhammad (S.A.W) alifanya biashara vizuri sana hata faida iliyopatikana ilikuwa zaidi kuliko alivyotumainia bi Khadija. Sifa alizoelezwa na mtumwa wake juu ya utukufu wa maisha na uaminifu wa Mtume (S.A.W) zilimfanya Bi Khadija kutaka kuwa mke wa mtu mkuu kama huyo. Kwa hivyo alimuomba Mtume Muhammad (S.A.W) amwoe, naye alikubali na akafanya hivyo. Wakati huo Bi Khadija (furaha ya Mungu iwe juu yake) alikuwa na umri wa miaka arobaini na Mtume Muhammad (S.A.W) alikuwa na miaka ishirini na mitano.

### Aliwaacha huru Watumwa

Kitendo cha kwanza alichofanya Bi Khadija baada ya kuolewa kilikuwa kumpa mumewe mali yake yote, pamoja na watumwa wake. Mtume Muhammad (S.A.W) mara moja aliwapa uhuru watumwa wote. Hivi akiwa na umri wa miaka ishirini na mitano alifanya jambo ambalo viongozi wa watu wenye umri mkubwa kumpita yeye walikuwa hawajaweza kufanya katika maisha yao marefu. Alionyesha ya kuwa iliwezekana kufanya kazi na kuishi bila ya watumwa katika mji ambako utumwa ulikuwa kila wakati ukifikiriwa ni jambo muhimu katika maisha.

## Maisha yake ya Ibada

Maovu yaliyoenea kati ya watu wa nchi yake yalimfanya Mtume Muhammad (S.A.W) kuwa na huzuni. Alizoea kwenda peke yake kwenye pango lilokuwa juu ya mlima unaoitwa Hiraa maili tatu kutoka Makka, na huko aliifikiria hali ya nchi yake, na kuabudu kwa masanamu ambako kulikuwa na nguvu. Ndani ya pango hili alimwabudu Mungu mmoja wa pekee na Mzima wa milele. Alipata nguvu nyingi katika kuabudu huku, ikawa mara nyingi alichukua chakula cha kutosha kwa siku kadhaa, na akapitisha muda mrefu katika pango hilo kwa kumwabudu Mungu.

Usiku mmoja katika mwezi wa Ramadhani, mwaka 609 A.D Mtume Muhammad (S.A.W) alipokuwa na Umri wa miaka arobaini, Malaika Jibril alitokea mbele yake alipokuwa akiabudu ndani ya hilo pango la Hiraa na akamwambia maneno haya.

'Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba. Yeye Kaumba mtu katika tone la damu. Soma na Mola wako ni Mtukufu kabisa Aliyefunza (kuandika) kwa kalamu. Yeye Kawafunza watu wasiyokuwa wakiyajua'. (Kurani Tukufu 96:6)

Siku hii ndiyo ya kwanza Mtume Muhammad (S.A.W) kujua kuwa yeye atakuwa mtume. Aliambiwa kwamba itakuwa ni kazi ya taabu kubwa kabisa. Ilimpasa kubadilisha tabia za watu kila pahali na kufundisha watu wote kuishi maisha yao kama Mungu Awatakavyo wao waishi. Kazi ngumu kabisa! Kwa sababu watu wakati huo walikuwa wamejaa maovu.

Ujumbe ambao aliambiwa na yule Malaika Jibril ulimshitusha sana Mtume Muhammad (S.A.W) hata ukamfanya amweleze Bi Khadija mambo yote, na kusema kwamba kwa njia hiyo

Mungu Alitaka kumjaribu. Khadija, ambaye alimjua vizuri kwa sababu alimpenda na alichunguza mienendo yake, alimfariji, na akasema: ‘Siyo, Mungu kwa hakika hatakufedhehesha, kwani wewe una huruma kwa jamaa zako, unawasaidia wasioweza kujisaidia, unawakaribisha wageni, na unawasaidia wale ambao wamo katika taabu. Alikuwa ni mkewe aliyesema haya na kila siku mke ndiye hakimu mzuri kabisa wa utu wa mume.

Mtume Muhammad (S.A.W) hata hivyo hakuridhika na maneno aliyosema mkewe, na kwahivyo mkewe akamnasihi aende kwa jamaa yake Waraqa-bin-Naufal, kipofu ambaye alikuwa mwanafunzi wa Biblia, na kumwuliza yeye maana ya ujumbe ambao Malaika Jibril alimletea.

Mtume Muhammad (S.A.W) alikwenda kwa Waraqa na kumweleza yote yaliyotokea. Hapo hapo Waraqa aliposikia hivi yeye alisema “Huyu ndiye Malaika, Mungu Aliyemshushia Musa” Tena Waraqa aliongeza: ‘Nasikitika mimi ni mzee. Natamani laiti ningelikuwa kijana “.watu watakapokufukuza kutoka katika maskani yako na ningekusaida sana.

Mtume Muhammad (S.A.W) alitumia muda mwingi wa maisha yake kufikiri namna gani ataweza kuwasaidia wale alioishi baina yao, na walimpenda. Kwahivyo yeye alistaajabu kuelezwa kuwa jamaa zake watamfukuzilia mbali. ‘Hakika jamaa zangu watanifukuza kwao na katika mji wangu? Mtume aliuliza. Waraqa alijibu: ‘Hakika watafanya hivyo. Kwani kila wakati mtu akiaminiwa na ujumbe kama wako, jamaa zake hawajamwamini na wamemtendea vibaya. yote ambayo Waraqa alimwambia Muhammad (S.A.W) yalimtaabisha na kumstaajabisha. Lakini kutakuwa mastaajabu makubwa zaidi juu yake.

## SURA YA NNE

### Kupewa utume

Baada ya miezi michache, Mungu tena alisema na Mtume Muhammad (S.A.W) akirudia amri kwamba yeye lazima kubadilisha tabia za watu kuwaita kuja kwa Mungu; kwamba ni lazima awaambie watu wasifanye dhambi za aina yoyote na kumwamini na kumwabudu Mungu Aliye mmoja. Na hivi Mtume Muhammad (S.A.W) akawa Mtume. Lakini mara ile alipokuwa mtume rafiki zake walimgeukia. Wale ambao walizoea kumsifu wakaanza kuleta matata juu yake.

### Abu Bakar kwenda pamoja naye

Walikuwapo watu wanne ambao waliendelea pamoja na Mtume Muhammad (S.A.W) na kumwamini mara moja. Walikuwa ni wanne waliomjua zaidi ya wote; Bi Khadija, mke wake; Hadhrat Ali ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi tu, mtoto wa Abu Talib, baba mdogo wa Mtume Muhammad (S.A.W) Hadhrat Zaid, mtumwa ambaye Mtume Muhammad (S.A.W) alimwacha huru; na Abu Bakar, rafiki yake aliyempenda sana. Watu hawa walimjua tangu siku zake za ujana na hawajapata kumsikia akisema uwongo. Kwahivyo, walisema, ilikuwa haiaminiki kwa yeye kudai kuwa ni mtume ikiwa yeye kwa hakika siye mtume halisi.

Siku ile ambayo Mungu Alisema na Mtume Muhammad (S.A.W) kumwambia kuwa Yeye Amemfanya Mtume Wake; Abu Bakar alikuwa amekaa katika nyumba ya mtu mkuu wa Makka. Msichana alikuja katika chumba akasema: “Nastaajabu ni jambo gani limempata Khadija leo! Anasema mumewe ni mtume kama Musa alivyokuwa mtume.” Hapo

watu wakacheka na kusema kwamba Khadija, ama Mtume Muhammad (S.A.W) lazima mmoja wao awe na wazimu. Lakini Abu Bakar alitoka huko nyumbani na kwenda kumtazama Mtume Muhammad (S.A.W) na kumwuliza je, yeye amedai kuwa ni mtume. Mtume Muhammad (S.A.W) akajibu kuwa Mungu Amemchagua yeye awe kiongozi wa watu, na kuwafunza kumwamini Mungu Mmoja tu.

Kusikia hivi Abu Bakar hakuuliza tena maswali, Bali alisema: 'Nasema kwa kweli, nikiapa kwa baba yangu na mama yangu, kuwa hujapata kusema uwongo hata mara moja na najua kwamba huwezi kusema lolote juu ya Mungu ambalo si kweli. Nashuhudia, kwahivyo, kwamba yupo Mungu Mmoja tu, na kwamba wewe ni mjumbe wa Mungu.'

Abu Bakar alikuwa na marafiki wengi ambao walimheshimu kwa sababu ya usafi wa maisha yake. Kati ya hawa walikuwako vijana kadhaa, na Abu Bakar akaanza kuwaambia mafunzo ya Mtume Muhammad (S.A.W). Kabla ya muda mrefu saba wa vijana hao walimkubali Mtume Muhammad (S.A.W) kuwa ni Mtume. Watano katika hawa saba walikuwa Uthman, Zubair, Abdur Rahman bin Auf, Sa'ad na Talha, watu wote hawa walikuwa na vyeo vikubwa. Wengine walioamini mbele walikuwa, Bilal, Yasir na mkewe Summaya na mtoto wake Ammar. Abdullah bin Masud, Khabbaa na Arqam. Nyumba ya mtu huyo aliyetajwa mwisho ilifanywa nyumba kuu ya mikutano kwa wafuasi wa Mtume Muhammad (S.A.W) kiasi cha miaka minne baada ya kupewa utume. Mnamo miaka mitatu tangu Mtume Muhammad (S.A.W) kupewa utume, watu ishirini walikuwa wafuasi wake.

## Mateso kwa imani yao

Si jambo rahisi kukubali ukweli. Wale Watu wa Makka ambao walijipatia riziki za maisha yao kama watunzaji wa makanisa ambako masanamu yaliabudiwa, hawakuweza kufikiriwa kumsikiliza mtu yeyote ambaye anafundisha watu kuabudu Mungu Aliye Mmoja. Kwahivyo jamaa wa wale walioongoka kuwa Waislamu walijaribu jinsi uwezo wao ulivyowawezesha kuwafanya hawa waongofu kuacha kumwamini Mungu Mmoja. Mikono na miguu ya Othman ilifungwa kwa kamba na mjomba wake aliyemfungia ndani ya chumba kimoja na kusema hatamwachilia huru mpaka aiache hiyo itikadi yake mpya. Kijana mwingine Mwislamu, Zubair ambaye umri wake ulikuwa miaka kumi na minne tu, alifungiwa ndani ya chumba, na jamaa zake wakakijaza chumba hicho “na moshi. Lakini Zubair alishikilia imani yake wala hakugeuza hiyo itikadi yake. Mama wa kijana mwingine Mwislamu alikataa kula chakula chochote mpaka mwanawe awe ametupilia mbali itikadi yake mpya na kurudia itikadi yake ya zamani ya watu wake. Mtoto huyu alijibu kuwa yeye yu tayari kuwatii wazazi wake katika kila jambo la kidunia, lakini siyo wakati wanapojitia katika kupinga matakwa ya Mungu.

Mtume mwenyewe hakuachiliwa. Siku moja alipokuwa amepiga magoti, na ameinamisha mgongo wake akisali katika Kaaba, Abu Jahli alichukua mtoto mchanga mchafu wa ngamia ambaye bado siku zake za kuzaliwa kutimu, na akamweka shingoni pa Mtume (S.A.W). Jinsi alivyokuwa na tabia ya kutoka nyumbani kwake alfajiri kwenda kusali, watu waliweka matawi ya miti ya miiba katika njia yake, ikawa katika giza alijiumiza kwa miiba hiyo. Mara nyingine watu walimtupia Mtume (S.A.W) mchanga na mawe. Siku moja kikundi cha Makureshi masharifu walimshambulia Mtume (S.A.W). Mmoja

wa Makureshi hao, Uqba-bin-abi-Muit, alirusha kilemba chake na kukizunguusha katika shingo ya Mtume (S.A.W) halafu kwa kukivuta kwa nguvu alikaza shingo hata ikawa maisha ya Mtume Muhammad (S.A.W) yaliokolewa na Abu Bakr akisema, “Mwataka kumwua mtu huyu kwa sababu anasema kuwa Mungu ni Mola wake?” Watu walijaribu kumwua Mtume (S.A.W) kwa njia nyingi.

**Njia yake ya kueneza Ujumbe wake**

Siku moja Muhammad (S.A.W) akisimama juu ya mlima wa Safaa, aliwaita watu kutoka koo kubwa kubwa za Makka kwenda kwake. Watu walimjua na walimwamini, kwahivyo walikusanyika na kumzunguka. ‘Mmepata kunisikia mimi nikisema uwongo? Mtume (S.A.W) aliwauliza. Wote walisema kuwa; walijua kila wakati alikuwa msema mkweli. Halafu aliwaambia, ‘Ikiwa nitawaambieni kwamba jeshi kubwa la askari limejificha nyuma ya mlima huu, tayari kukushambulieni, mtaweza kunisadiki?’ Hata katika siku hizo ilielekea kuwa haikuwezekana kamwe kuwa jeshi lolote laweza kuhujumu. Zaidi ya hivi, wachungaji walizoea kulisha ngamia na mbuzi wao kila upande kuzunguka Makka, kwa hivyo ikiwa jeshi lolote lilijongea kuhujumu mji huo, wachungaji hawa waliweza kurejea mbio na kuletea wenyeji habari za kujongea kwa jeshi hilo. Ingawa hivyo watu wote walimjibu Mtume Muhammad (S.A.W) kuwa bila, shaka wataweza kumuamini, kwa sababu hawajapata kumsikia akisema uwongo. Kwa hivyo sasa Mtume (S.A.W) aliwaambia: Mwasema kuwa, sijapata kusema jambo lisilokuwa la kweli. Vizuri sana, hivyo! Sasa nakuambieni kuwa Mungu Amenichagua mimi kueneza ujumbe Wake kwenu ninyi, na kukuonyesheni nyinyi mnafanya dhambi katika mienendo yenu.’ Lakini aliposema maneno hayo, wote

waliohudhuria walikasirika sana, na kukimbia. Kwa kusema kwamba lazima awe ni mwenye wazimu au amejidai.

### Mateso zaidi kwa wafuasi wake

Kisa cha mkutano huu kilipohadithiwa katika Makka wafuasi wa Mtume (S.A.W) walianza kuteswa zaidi kushinda hapo mbele. Mtu mmoja alikataa kuwa na jambo lolote kuhusiana na ndugu yake ambaye alikuwa amesilimu. Wazazi waliwafukuza watoto wao kutoka nyumbani kwao. Watumwa walitendewa kikatili sana na mabwana zao. Vijana ambao walipendelea ukweli kuliko desturi za watu wa zamani, na ambao walikuwa wepesi kukubali mafunzo ya Mtume Muhammad (S.A.W) walipelekwa gerezani, na kuwekwa huko bila chakula, na wazee wao. Lakini waliendelea kumwabudu Mungu na midomo mikavu na macho ya uchovu. Baadhi ya wazazi hao ambao waliogopa watoto wao waweza kufa, mwishowe waliwapa chakula. Lakini hapana mtu aliyeonyesha huruma kwa watumwa na watu maskini walioongoka kuwa Waislamu. Watumwa walilazimishwa kuvaa nguo za chuma za kivita na kusimama katika jua kali mpaka ngozi zao zichomeke vibaya kwa moto. Baadhi yao walikokotwa kwenye mchanga wa moto kwa kamba zilizofungwa miguuni mwao. Miili ya wengine ilichomwa kwa chuma cha moto kabisa kilichokuwa chekundu kwa moto. Wengine walitiwa pini zenye ncha kali katika ngozi zao. Bibi mmoja mwema Mwislamu aliuwawa kwa aibu sana kwa mkuki aliochomwa kutoka upande mmoja wa mwili wake mpaka kutokea upande wa pili. Mwanamume mmoja aliyeitwa Omar alizoea kumpiga mtumishi wake msichana, aliyeitwa Lubaina mpaka mwenyewe alipochoka. Baada ya kuchoka alimwambia Lubaina, “Sasa naacha kukupiga, si kwa sababu nakusikitikia,

bali kwa sababu nimechoka sana kuendelea kukupiga”. Lakini Omar mwenyewe baadaye aliongoka na kuwa Mwislamu.

Tumeisha wataja Bilal, Yasir, mkewe Sumayya na mtoto wake Ammaar ambao walikuwa katika kundi la wafuasi wa kwanza wa Mtume (S.A.W).

Bilal alikuwa mtumwa wa Kihabeshi, Bwana wake alimlaza chini ardhini, jua kali sana la mchana likamwangazia. Halafu mawe mazito yaliwekwa juu ya kifua chake. Lakini katika maumivu yote hayo Bilal (furaha ya Mungu iwe juu yake) aliendelea kusema, ‘Yupo Mungu mmoja tu’. Baba na mama wa Ammaar waliteswa sana. Miguu ya Yasir ilifungwa kwa ngamia wawili, kila mguu kwa ngamia mmoja; ngamia hao walielekezwa pande mbalimbali na Yasir (furaha ya Mungu iwe juu yake) alichanika vipande vipande. Sumayya aliuawa kwa njia mbaya zaidi. Mambo mengine, mabaya sana kuelezwa, walifanyiwa wale waliomfuata Mtume (S.A.W). Lakini Waislamu hawa mashujaa hawakuitupa itikadi yao katika Mungu mmoja wa kweli. Walikubali kufa kuliko kufanya hivyo, na wengi walikufa baada ya kuteswa sana ajabu. (Furaha ya Mungu iwe juu yao wote). Watu wa Makka wenyewe walistaajabia ushujaa wa watu hawa. Lakini ukatili wao hawakuacha; wakawa hata wabaya kupita walivyokuwa mwanzoni.

## SURA YA TANO

### Mafunzo ya Mtume

Pasipo kujali matata haya Mtume mtukufu (S.A.W) aliendelea na mafundisho yake. Kila pahali alipoona watu wachache wamekaa pamoja alikwenda na kuwaeleza habari juu ya Mungu. Aliwafundisha kwamba kuna Mungu mmoja tu; hana mtoto wa kiume wala wa kike; hana baba wala mama. Wao lazima wamkubali na kumwamini na kumwabudu Yeye tu. Mungu hana upungufu wowote. Aliiumba dunia, Ana uwezo wote. Hawezi kuonekana na macho ya binadamu. Roho za wafu wanaokufa hurejea Kwake na hupewa maisha mapya. Kwa hivyo watu wote inawapasa kumpenda na kujaribu kukaribiana na Yeye. Yawapasa kusafisha nyoyo zao na kuongoza vema ndimi zao na vitendo vyao. Wasitumie nyakati zao kwa kutafuta utajiri, au kwa kutosheleza matakwa yao. Yawapasa wafanye kazi kwa ajili ya watu, na wajaribu kueneza mapenzi na amani katika dunia. Yote haya yalifunzwa na Mtume Muhammad (S.A.W). Hata hivyo watu walimcheka.

### Itikadi za watu wa nchi yake

Watu wa Makka walikuwa ni wenye kuabudu masanamu na makanisa yao yalikuwa na mamia ya masanamu ambayo waliyaabudu na kuyatolea sadaka. Sadaka hizo zilikuwa ni mali ya watunzaji wa makanisa hayo, baada ya kumaliza sherehe ya masanamu.

Jambo kubwa katika itikadi ya watu wa Makka lilikuwa kwamba Mungu Amewapa miungu wengine uwezo wa kulinda dunia, na kwamba uwezo wa kuponyesha wagonjwa, kuwapa watoto wale wasio na watoto na kuondosha njaa ulikuwa katika

mikono ya miungu hawa; na kwamba hakuna msaada ulioweza kupatikana kutoka kwa Mungu mpaka kwanza uwe umeulizwa masanamu hayo waliyoyaabudu. Watu wa Makka waliomba haja zao kutoka kwa miungu hao waliowasadiki kwa kujitupa chini na kulala kifudifudi mbele ya masanamu haya, kutembea wakiyazunguka na kutoa sadaka za wanyama na mazao ya mashamba yao. Pamoja na masanamu hayo, jua, mwezi na nyota vilifikiriwa kuwa na uwezo wa kutoa msaada ikiwa viliabudiwa, pia watu waliabudu vipande vya mawe, miti na mafungu ya mchanga. Walifikiri kuwa malaika ni watoto wa kike wa Mungu.

Kwa watu wenye itikadi ya namna hii, fikra ya kuwa kuna Mungu Mmoja tu ilionekana kuwa ni ujinga mkubwa. Walikuwako wengine ambao walikuwa hawaamini Mungu kabisa, au maisha ya baada ya kufa, au katika siku ya Kiyama.

## Kazi Yake ya ajabu

Haistaajabishi kuwa Mtume Mtukufu (S.A.W) aliona Kazi aliyopewa na Mungu ni ngumu sana. Ingawa hivyo, katika muda mfupi wa miaka ishirini Mtume Muhammad (S.A.W) aliweza kukomesha ibada ya masanamu katika Bara Arabu. Pamoja na Waarabu walijifunza kutoka kwake itikadi ya Mungu Mmoja na itikadi hii ikaenea katika dunia nzima. Kama dunia ilivyojulikana siku hizo kwa ajili ya kuheshimu jina la Mungu.


Katika wakati wa Mtume Muhammad (S.A.W), kulikuwa hakuna serikali ya ushirika wa majimbo yote ya nchi hiyo ya kuweka hali nzuri ya daima katika Bara Arabu. Nchi yote ilikuwa imegawanyika katika majimbo madogo madogo. Watu wa jimbo moja walizoea kugombana na wale wa jimbo jingine, na ugomvi huu ulikuwa ukidumu kwa miaka mingi sana. Mambo madogo kama neno la tusi, au kijikosa kidogo

kinachotokea katika mashindano ya farasi, kiliweza kuleta vifo vya maelfu, na watu kuchukuliwa kupelekwa utumwani baada ya kuchukuliwa kama mahabusu. Ni watu wa aina hii ambao Mtume mtukufu (S.A.W) aliwageuza kuwa ndugu Waislamu.

Maisha ya watu wa Makka yalikuwa na mambo mengi mabaya. Kunywa pombe, kucheza kamari kwa pesa, na itikadi ya uchawi yalikuwa baadhi ya mambo hayo. Ulevi ulipewa watu kunywa mara kadhaa kila siku katika nyumba zote. Lakini wakati ule ule Kurani Tukufu ilipokataza kunywa pombe, hata vyombo vya kuchukulia pombe vilivunjwa vipande vipande. Siku hiyo pombe ilitiririka katika barabara za Madina kama maji ya mvua.

**Itikadi katika ushirikina**

Katika nyakati hizo waarahu hawakuwa na ujuzi mwingi. Wachache tu waliweza kusoma ama kuandika kwa kuwa walikuwa na ujuzi kidogo, watu walikuwa wakiamini namna nyingi za mambo ya kustaajabisha. Walifikiri kuwa mashetani wanaishi mahali pao peke yao, na wanaeneza magonjwa ya namna nyingi mbalimbali. Kuepukana na kupata magonjwa hayo, watu walijaribu kuwafurahisha mashetani hao kwa



**Ka'ba**

nyimbo za ajabu na kucheza ngoma. Watu waliwasadiki wale watu ambao walijidai kuwa wanaweza kung'amua mambo yatakayotokea nyakati zijazo. Katika muda wa miaka michache Mtume Muhammad (S.A.W) aliwatoa Waarabu wote kutokana na desturi na itikadi zao za zamani.

**Hali ya wanawake**

Wanawake walifikiriwa kuwa si watu wa maana hata kidogo na mahali pao katika jamii ya watu palikuwa pa nyuma na pa kudharauliwa hasa. Jinsi walivyotendewa haikuwa bora hata kuliko wanyama. Mwanamke alifikiriwa tu kuwa ni sehemu ya mali ya mtu. Ikiwa mumewe, au mtu wa ukoo wake mwingine alikufa, mwanamke alikuwa hana haki ya kupata sehemu yoyote ya mali yake. Hakika, mwanamke mwenyewe alikuwa akifikiriwa kuwa ni sehemu ya mali ya mumewe aliyekufa, na mrithi wa mumewe aliweza kufanya alilopenda naye. Aliweza kumwoa mwenyewe au kumwoza mtu yeyote mwingine awaye.

Baadhi ya wanawake walikuwa na waume zaidi ya mmoja, na mume aliweza kuwa na wake wengi sana kama alivyopenda.

Tukifikiri hali hiyo mbaya sana ya wanawake katika Waarabu, wanawake wa siku hizi lazima wamshukuru Mtume Muhammad (S.A.W) aliyewanyanyua kutoka hali ya kudharauliwa kabisa mpaka katika hali ya kuheshimiwa. Ni yeye aliyewaambia wanaume 'Mbora kati yenu ni yule anayemfanyia mkewe mema sana.' Na Kurani Tukufu yasema juu ya wanawake (2:229): "Wanawake wanayo haki sawa na ile iliyo juu yao wanaume kwa sheria". Mke kwa mintarafu ya mali, ana haki kama mume wake. Aweza kufanya apendavyo na pesa zake, bila ya kumwuliza mumewe.

## SURA YA SITA

### Kuhamia Uhabeshi

Katika mwaka wa tano baada ya Mtume mtukufu (S.A.W) kuchaguliwa na Mungu kufanya kazi yake kubwa ajabu, Mtume (S.A.W) alikuwa amekwishakusanya kundi la watu zaidi ya hamsini kama marafiki wa karibu kabisa. Mateso waliyokuwa wakifanyiwa hawa wafuasi wake yaliwaongeza moyo wa kuimarisha ujamaa wao zaidi. Mtume (S.A.W) alikuwa mtu wa huruma sana, na hata hakustahamili kuona maumivu ya watu wengine hata kama ni maadui zake. Kila wakati alijaa huzuni kuwaona katika hali hiyo. Basi hivi angewezaje kustahmili kuona maumivu ya rafiki zake waliposumbuliwa na maadui zao? Marafiki hao walimsaidia Mtume sana; alimhitaji kila mmoja wa hao marafiki. Hata hivyo alipoona kuwa maadui kila siku, wanazidi kuwa wakali, aliwashauri Waislamu watoke hapo, na waende mahali penye usalama. Hakuwa akijiogopea nafsi yake, lakini hakuweza kustahmili kuona rafiki zake wakitendewa ukatili mwingi hivyo. Aliwashauri waende Uhabeshi ambako kulikuwa kukitawaliwa na mfalme wa Kikristo aliyeitwa Najjashi. Waislamu wengi wanaume na wanawake waliacha makao yao katika Makka na kwenda Uhabeshi. Hata huko hawakuweza kuepukana na hamaki za watu wa Makka. Mfalme wa Uhabeshi alipokea baadhi ya watu ambao walipeleka ujumbe wa kutaka Waislamu warejeshwe katika mji wao wa Makka. Lakini mfalme huyu Mkristo alikuwa ni mfalme ambaye alipenda kufanya uadilifu. Alipousikia ujumbe, alitaka kuwasikia Waislamu walikuwa na maneno gani ya kusema juu ya jambo hili, kwa hivyo waliletwa mbele yake. Mfalme aliwauliza kwa nini walikuja katika nchi yake. Hapo mmoja kati yao, Ja'far bin Abi Talib, alisimama akasema: 'E Mfalme! Sisi tulikuwa watu wajinga, tuliabudu masanamu.

Tulikuwa wala mizoga, na kufanya kila namna ya mambo maovu. Tulikuwa hatuna adabu kama itupasavyo kwa jamaa zetu, na tuliwatendea mabaya majirani zetu. Sisi ambao tulikuwa wenye nguvu tuliwanyang'anya waliokuwa wanyonge kwa kutajirika. Mwishowe Mungu Katuletea Mtume (S.A.W) kuja kutugeuza tuache mabaya tuyafanyayo. Maisha mema ya Mtume (S.A.W) yanajulikana sana na sisi. Alituita kujiunga katika kuabudu Mungu mmoja tu, na kuacha kuabudu masanamu na mawe. Alituambia daima tuseme ukweli, kila wakati tufanye mambo yanayotupasa kufanya, kuwastahi jamaa zetu na kufanya yaliyo mema kwa watu wote. Alitufunza tuepukane na kuua na kila namna ya mambo machafu. Alitukataza kutumia mali ya mayatima bila idhini ya sheria, au kutamka maneno yasiyokuwa ya heshima kuhusu wanawake. Kwahivyo tulimwamini, na kumfuata na kutenda kama mafunzo yake yalivyotuagiza. Ndipo watu wetu wenyewe walianza kutufanyia mabaya. Wao walitutaabisha wakifikiri kuwa sisi twaweza kuacha itikadi yetu katika Mungu mmoja na turejee katika kuabudu masanamu. Wakati ukatili wao ulipozidi kiasi hata tukashindwa kuustahimili, tulikuja kutafuta pahali pa usalama katika nchi yako ambako tunatumaini kuwa hakuna dhara inayoweza kutupata.

Mfalme alipendezwa sana na hotuba hii hata akakataa kuwapa watu wa Makka Waislamu. Halafu baadaye watu wa Makka waliwaendea masharifu ambao walikuwa wanachama wa baraza la mfalme. Waliwapa hao masharifu pesa na kufanya mipango ya siri pamoja nao ya kuwaendea Waislamu kichinichini, kwa kusema kwamba Waislamu wamezoea kusema mambo mabaya kumhusu Nabii Isa. Mfalme tena aliwaita Waislamu na kuwauliza wanafikiri nini juu ya Nabii Isa.Waislamu walimweleza Uislamu unavyofunza juu ya Nabii Isa, kuwa yeye alikuwa mtumishi mpenzi wa Mungu na ni

mtume. Walikuwa hawawezi kukubali kuwa ni Mungu kwa sababu Mungu ni Mmoja. Jambo hili liliwakasirisha sana hao masharifu na kumwambia Mfalme awaadhibishe Waislamu kwa sababu hiyo. Lakini Mfalme alisema: Kwa mujibu wa itikadi yangu mwenyewe pia, Isa hakuwa zaidi ya hivyo Waislamu walivyosema.Aliwaeleza masharifu kuwa hakuzijali hamaki zao. kwa sababu yeye bora amfurahishe Mungu kuliko kuwa mfalme wa nchi yake. Alikataa kuwatoa Waislamu kuwapa maadui zao.

**Nyakati mbaya katika Makka**

Katika Makka mashambulio kwa Mtume mtukufu (S.A.W) mwenyewe yalizidi. Baba yake mdogo, Abu Talib, ambaye alikuwa ni mmoja wa wakuu wa mji huo na ambaye ndiye alikuwa akimlinda Mtume (S.A.W) mahali pa wazazi wake waliokuwa wamekufa, siku moja aliombwa na watu wa Makka kumzuia Mtume (S.A.W) kufundisha. Halafu baadaye walimuomba jambo kubwa sana zaidi. Walimwomba amchukue nyumbani kwake mtoto wa mtu mwingine mkubwa, na kumpa huyo kijana mpya kila kitu alichokuwa nacho, naye amchukue Mtume Muhammad (SA W) na kuwapa watu hawa wa Makka, ili waweze kutenda naye jambo lolote walilotaka. 'Hili kwa hakika ni ombi la ajabu sana'; alijibu Abu Talib, Ninyi mwanitaka mimi nimpe mmoja wa watoto wenu, mali yangu yote, na niwape mtoto wa ndugu yangu mumtese. pengine auwawe nanyi? Hata mnyama anaweza kumwua mtoto wake na kumpenda wa mwenzie?

Wa-Makka walivunjika moyo kwa jibu hilo. ndipo wakamwomba Abu Talib kumzuia mtoto wa ndugu yake asihubiri juu ya Mungu Mmoja na ubaya wa kuabudu masanamu. Abu Talib alimwita Mtume Muhammad (S.A.W)

na kumwomba ikiwa ataweza kuwaridhisha watu wakubwa wa Makka kwa kufanya walivyotaka. Mtume Muhammad (S.A.W) alijibu, “Amin, nina mengi ya kukushukuru juu yake, na ningependa kukufurahisha, lakini hata kwa ajili yako siwezi kufanya jambo hili. Ikiwa wewe waogopa hamaki za watu, niachilie nafsi yangu. Lazima nihubiri ukweli ambao Mungu Amenifunulia mimi. Siwezi kunyamaza kimya na kuangalia watu wangu wakielekea kule kwenye hatari”.

Mwishoni watu wa Makka walijaribu kumsemesha Mtume (S.A.W) mwenyewe. Walimtuma mzee mmoja kumwomba asiharibu amani ya mji, na kumweleza kuwa ikiwa sababu ya kufanya hivyo alivyokuwa akitenda ni kuwa anataka kupata sifa au utajiri, wao wako tayari kumpa yote mawili. Ikiwa yeye anataka kuwa mfalme wao wako tayari kumkubali kama mfalme; na ikiwa anataka kupata mke, basi, anaweza kuchagua mmoja katika wasichana wote wa Makka. Lakini lazima yeye aache kabisa kufundisha kuwa kuna Mungu Mmoja tu. Mtume mtukufu (S.A.W) alijibu, “Hata ukiweka jua katika mkono wangu wa kulia na mwezi katika mkono wangu wa kushoto sitaacha kueneza ukweli. Nitaendelea katika njia hii mpaka nifaulu ama nife katika juhudi hii. Katika wakati huo ni watu themanini waliokuwa wameingia katika kundi la Mtume (S.A.W).

Watu waliokuwa wakiishi katika vijiji vilivyozunguka walisikia matata yaliyokuwa Makka wakasafiri kwenda huko kutazama wenyewe ni jambo gani na kuona mambo yaliyolihusu. Watu wa Makka walihamaki kwa kitendo hiki cha wana-vijiji, na kwa hivyo amri ikatolewa kuwa watu wazuiliwe kumuona Mtume mtukufu (S.A.W). Katika wakati huo walikata shauri kumwua. Walipopata habari hii baba yake mdogo Mtume (S.A.W) na jamaa zake wengine walimchukua wakampeleka katika bonde

lililokuwa karibu ambako kulikuwa na usalama bora zaidi. Tena watu wa Makka walijaribu njia nyingine. Walitoa amri kuwa hapana mtu kuuza aina yoyote ya nguo au chakula kwa Mtume Muhammad (S.A.W) au kwa mtu yeyote wa ukoo wake au kwa Mwislamu mwingine. Hawa waliotajwa walikuwa hawana ruhusa kuoa au kuwa na uhusiano wowote na watu wa Makka. Amri hizi zote zilikuwa lazima kufuatwa kwa uthabiti, mpaka Waislamu walazimike kumweka Mtume mtukufu (S.A.W) mikononi mwa watu wa Makka. (Makka ni mji katika jangwa, maili arobaini kutoka katika mji wowote mwingine. Kwahivyo yaweza kufikiriwa jinsi Waislamu walivyoteseka kwa njaa na kukosa mavazi. Mara nyingi iliwabidi kuishi kwa siku nyingi kwa chakula cha majani na, magome ya miti). Kwa miaka mitatu kamili, Mtume Muhammad (S.A.W) aliteseka kwa njia hii kwa sababu ya kuwahubiri watu kuwa yawapasa kumwabudu Mungu Mmoja. lakini kuteseka kwake yeye na wapenzi wake hakukumgeuza na kumtoa katika kazi yake ya heshima na utukufu.

Mwisho wa miaka mitatu hiyo baadhi ya watu wa Makka walichoka kumtesa Mtume mtukufu (S.A.W) na walimwachilia yeye na wafuasi wake (Waislam) watoke katika bonde. Lakini baba mdogo wa Mtume (S.A.W) aliyekuwa mzee na mkewe mwaminifu walikuwa wameathirika sana kwa muda huo mrefu wa miaka mitatu ya kuteswa, kwahivyo walikufa muda mdogo baada ya hiyo miaka mitatu.

## SURA YA SABA

### Safari ya kwenda Taif

Kwa kuona kwamba watu wa Makka hawasikilizi mafunzo yake, Mtume (S.A.W) alifikiri kwamba ingefaa kujaribu miji mingine ya Bara Arabu, na kwahivyo alisafiri kwenda Taif, mji uliojengwa zamani, umbali wa maili arobaini kutoka Makka. Mtume (S.A.W) alijaribu kuwahubiria watu wa Taif juu ya Mungu Mmoja, walitokea kuwa ni wakatili hata kuliko watu wa Makka. Walimchekelea na kumwita majina mabaya na baadaye kumfukuza kutoka mji wao. Walimtomeshea mbwa zao na kumtupia mawe ambayo yalimwumiza na kumfanya atokwe na damu. Mtume Muhammad (S.A.W) aliendelea na mwendo wake na huku akijifuta damu, akimwomba Mungu kwa maneno haya: “Mola, watu hawa hawajui kwamba ninayowaambia ndiyo kweli, wanafanya hivi kwa sababu wao wanaflkiri ni vizuri kutenda hivyo. Usiwakasirikie, na usiwaadhibu, bali wafunue macho yao waone ukweli na uwasaidie kuukiri”. Ni mapenzi gani yaliyoonyeshwa badala ya ukatili mkubwa huo! Mfano ung’aao ulioje wa mapenzi juu ya wanadamu wote! Pamoja na hayo maneno haya yatupa mwangaza mkubwa kwenye ukweli wa, itikadi ya Mtume (S.A.W) kwamba alitumwa na Mungu na pia kwa nguvu za utu wake. Mtu mmoja asiyekuwa jamaa yeyote anaendelea mbele kwa jina la Mungu, kuwaita watu wamwabudu Mungu!

### Kuenea kwa Uislam Madina

Ukweli hauwezi kuwekwa chini. Maelezo ya mafundisho ya Mtume (S.A.W) yalianza kuenea katika nchi yote. Baadhi ya watu wa madina walikwenda Makka kwa hija ya kila mwaka, walionana na Mtume Muhammad (S.A.W) naye akawaeleza mafunzo ya Islam. Walipendezwa sana na walikiri Uislam.

Waliporejea Madina watu hao waliwasimulia watu wa mji wao habari za Uislam. Mwaka uliofuata watu wengi zaidi walimtembelea Mtume (S.A.W) na wote walikubali Uislam. Walimwomba Mtume ahamie Madina na afanye mji huo kuwa maskani yake. Mtume (S.A.W) aliwajibu kuwa wakati wake wa kutoka Makka haujafika, lakini aliwaahidi kuwa atakwenda huko baadaye.

**Kuhamia Madina**

Mwaka wa kumi na nne tangu Mtume (S.A.W) kupewa utume sasa ulianza, naye pamoja na Abu Bakr na Ali walibaki peke yao Makka katika maadui zake. Wafuasi wake wengine walikuwa wameaga makwao kwa amri yake na wakaenda kuhitaji usalama Uhabeshi au Madina. Mara nyingi Abu-Bakar alimwomba aende Madina lakini Mtume (S.A.W) wakati wote alimjibu kuwa Mungu bado hajamwamuru kufanya hivyo. Nia ya Mungu bado ilikuwa Haijadhihiri kwa Mtume. Mpaka wakati huo kila namna ya majaribio ya kumwua yalikuwa yamefanywa na mtu mmoja mmoja tu, na kila jaribio halikufaulu. Kila aina ya kumtesa ilikuwa imejaribiwa, lakini tone moja bado lilikuwa halijatiwa kujaza kikombe cha vitendo viovu vya watu wa Makka. Mwisho saa ilifika. Wakamkuta Mtume (S.A.W) akielekea kuwa peke yake kabisa. Wakubwa wa Kikureishi walifanya mkutano katika Dar-un-Nadwa, ambako mambo ya kiserikali yalifikiriwa na mashauri kukatwa. Walikutana huko na kushauriana jambo gani afanyiwe. Baadhi yao walifikiri afungwe kamba na atupwe katika chumba cha giza na aachwe bila ya chakula mpaka afe. Wengine walifikiri asafirishwe mbali sana. Lakini mwishowe Abu Jahl alitoa mawazo yake kwamba vijana wa ukoo mkuu wapewe panga kali, nao hawa wote watamshambulia wakati mmoja, ili pasiwe na kabila maalumu la Makureshi la kushtakiwa kwa kuua. Banu Hashim - Kabila

la Mtume (S.A.W) lingeridhika. kwahivyo kupewa pesa za damu (fidia) badala ya kuwaadhibu wauwaji. Mpango huu ulikubaliwa na watu wote.

Wakati huo, mpango huo mbaya wa Makureshi ulijulishwa kwa Mtume (S.A.W) na Mungu. Mjumbe wa Mungu alimwambia Mtume (S.A.W) asilale katika kitanda chake usiku huo. Kwa hivyo Mtume Muhammad (S.A.W) alimwita Ali, na kumpa habari ya amri ya Mungu, na kumwambia jinsi atakavyoweza kutenda ili kuuharibu mpango wa Makureshi. Usiku ule Ali lazima alale penye kitanda cha Mtume (S.A.W). Hadhrat Ali baadaye atamfuata Mtume (S.A.W) Madina, ambako Mtume (S.A.W) atakimbilia. Lakini Ali pia kabla ya kuanza safari ya kumfuata alipewa kazi ya kuwapa watu vitu ambavyo Mtume (S.A.W) alikuwa akiwawekea kwa uaminifu. Hii yaonyesha jinsi watu walivyokuwa na staha kubwa kwa uaminifu huo usio na kifani na tabia njema za Mtume (S.A.W) hata ikawa kwamba ingawa nyoyo za watu zilimchukia alikuwa akiaminiwa kuweka kwa usalama kabisa mali zao. Kwa hivyo Mtume (S.A.W) alimwambia Ali (furaha ya Mungu iwe juu yake) kubaki na kufanya kazi hiyo, na Abu Bakar (furaha ya Mungu iwe juu yake) aliambiwa apange mipango iliyohusu safari ya kukimbilia Madina: kwa sababu Mungu kesha Amrisha iwe hivyo.

Baada ya giza kuingia, watu walio na silaha, Waliochaguliwa katika makabila ya Kikureishi, walijipanga nje ya nyumba ya Mtume (S.A.W) tayari kumhujumu mara akitoka nje. Mtume (S.A.W) alipoona giza la kutosha, na akiamini yuko katika himaya ya mikono ya Mungu, Ambaye katika miaka kumi na mitatu hiyo yote Alikuwa Amemlinda na adui zake. taratibu alitoka nyumbani kwake na kuanza safari ya kwenda Madina na akafika kwenye pango la Thaur, maili tatu kutoka Makka, pamoja na Abu Bakar.

Siku hiyo ya kwenda Madina ni siku kubwa katika historia ya Uislam kwa sababu mwaka wa Kiislam wa kalenda ya Hijra yaanza tangu siku hiyo.

Alfajiri ya pili, Makureshi walistaajabu kumwona Ali Akitoka kitandani. Kutafutwa kwa hadhari kulifanywa kila mahali na zawadi kubwa zilitolewa. Baadhi ya watafutaji walifuata alama za miguu ya Mtume (S.A.W) na Abu Bakar, na wakafika mpaka katika mahali pa kuingia pangoni. Abu Bakar (furaha ya Mungu iwe juu yake), kusikia sauti ya miguu yao, alihuzunika sana, si kwa ajili yake, bali kwa yule ambaye maisha yake, kwake, yalikuwa ghali zaidi kuliko yake mwenyewe. Ulikuwa ni wakati wa kuhangaisha sana. Kama maadui wangetazama tu ndani ya pango hilo, Mtume (S.A.W) na Abu Bakar wangekatwa katwa vipande. Lakini kuamini kwao katika nguvu ya mikono yenye nguvu ya ulinzi wa Mungu kuliwaokoa. Hata katika muda huu ambapo mambo yalikuwa mabaya sana. Moyo wa Mtume (S.A.W) ulikuwa katika utulivu kabisa wala haukuwa na woga.



**Mji wa Madina**

‘Usihuzunike, hakika Mungu Yupo pamoja nasi’ (Kurani Tukufu 9:40). Mtume (S.A.W) alimwambia rafiki yake! na kumtuliza hofu yake. Hakika hii haingeweza kuwa sauti kutoka kwa Mtume (S.A.W)! Kwa sababu moyo wa mwanadamu, kama alivyokuwa Mtume (S.A.W) haungeweza wenyewe kuwa katika utulivu katika wakati wa hatari kubwa. Ilikuwa sauti, iliyotoka juu, kwa Mungu. Bwana wa vyote, iliyokuja kumfariji na kuujaza amani moyo ambao uliteseka kwa ajili Yake.

Kwa siku tatu walikaa katika pango hilo. Mtoto wa Abu Bakr alikuwa akiwaletea habari ya mambo yote yaliyotendeka mjini. Mwishowe kutafuta kulikwisha, na mambo yalipokuwa timamu, walitoka nje ya pango siku ya nne. Mtume (S.A.W) na rafiki yake walifika Madina baada ya siku nane, na ilikuwa tarehe 12 Rabi-ul-Awwal, walipowasili huko, yaani katika mwaka wa 14 tangu Mtume Muhammad (S.A.W) kupewa utume. (Tarehe 28 Juni, A.D. 622)[1]

Habari kuwa Mtume (S.A.W) ametoka Makka zilifika Madina kabla yao. Watu katika mji huo walikuwa wakimngoja kwa hamu awasili. Kila asubuhi watu wengi walitoka na kwenda safari kidogo kwenye barabara ya kwenda Makka wakitumaini kumwona Bwana wao akitokea. Mwishowe siku ndefu za kungoja zilikwisha. Watu walitoka wamevalia mavazi yao mazuri sana, kuja kumlaki. Wanawake walipanda juu ya majumba yao kumwangalia. Kila mmoja alipenda Mtume aingie nyumbani kwake na kukaa huko. Lakini yeye aliliambia

---

1 *Baadhi ya wataalamu wamesema Mtume (SAW) alihama* ***Makka*** *katika mwezi wa Julai, na wengine wamesema ni mwezi wa Mei.*

kundi hilo la watu waliokuwa na furaha kuu lililomzunguka kwamba ataishi pahali popote ambapo ngamia wake atasimama. Alimwachilia ngamia wake kwenda popote alipopenda. Ngamia alikwenda mpaka katika uwanja uliokuwa mbele ya nyumba ya Abu Ayyub. Hapo alisimama.

Uwanja huo mbele ya nyumba ulikuwa ni wa watoto wawili ambao walikuwa mayatima. Walikubali kutoa bure uwanja huo kwa ajili ya kutumiwa kwa kujenga msikiti, lakini Mtume (S.A.W) hakupenda kuuchukua bila ya kuulipia. Wao, kwahivyo walikubali kulipwa thamani yake. Jambo lililofuata lilikuwa kujenga msikiti. Hii ndiyo kazi ya kwanza ya Mtume (S.A.W) baada ya kufika Madina. Naye pamoja na marafiki zake waliujenga msikiti huo kwa mikono yao. Wafanyakazi wote walijenga bila ya kutaka malipo. Walipokuwa wakijenga waliomba pamoja na Mtume (S.A.W), "E Mola! Hapana raha isipokuwa raha ya maisha baada ya kifo; Wasaidie wasaidizi na wakimbizi wanaohitaji msaada". Halafu Mtume (S.A.W) alifikiri jinsi gani kuwalinda wale watu waliokuja Madina kutoka Makka. Wengi kati yao walikuwa wakiishi maisha ya raha na ya kitajiri katika Makka, lakini walilazimika kuacha mali yao na utajiri wao nyuma. Kwa hivyo Mtume (S.A.W) alifanya udugu baina ya wasaidizi - Waislamu wa Madina - na wakimbizi waliotoka Makka. Kila mmoja katika wasaidizi alimchukua nyumbani kwake ndugu mmoja katika wale wakimbizi, na kutumia nyumba pamoja naye na pia kugawana naye nusu sawasawa ya kila kilichokuwa mali yake.

## SURA YA NANE

### Mtume kuchaguliwa mfalme wa Madina.

Watu wa Madina walikubali upesi mno mafundisho ya Mtume (S.A.W) na baada ya muda mfupi karibu wote walikuwa Waislamu. Walimchagua Mtume (S.A.W) kuwa mfalme wao. Mayahudi walikuwa miongoni mwao. Hivi jiwe ambalo waashi wa mji wake (Makka) walilitupa lilifanywa kuwa ndilo taji la mji wa Madina. Kama Mfalme wa Madina, pia aliwafunza watu juu ya kuabudu Mungu Mmoja, kuwaonyesha watu namna ya kuishi Kiislam.

### Vita vya Mtume (S.A.W)

Hakuna ukweli katika hadithi zilizotolewa juu ya Mtume (S.A.W) kuwa, alihubiri dini yake kwa upanga. Yeye aliweka msingi wa amani ya kudumu milele. Kwa kuwa alifundisha kuwa wanadamu wawe na mapenzi na heshima kwa waanzishaji wa dini zote kubwa za dunia, bali ni lazima kuwaamini hao. Kurani Tukufu imejaa maelezo yanayoonyesha kwamba kuamini dini hii au ile ni jambo linalomhusu mtu mwenyewe. Kila mtu ana uhuru wa kuchagua dini. Ikiwa anaukubali ukweli ni kwa wema wake mwenyewe, ikiwa hakubali ni hasara yake mwenyewe na kujiumiza. Kurani Tukufu yasema: ‘Hapana karaha katika dini’ (2:256). Ndiyo kusema hapana haja ya mtu kumlazimisha mwingine kufuata dini asiyotaka kufuata. Basi Mtume (S.A.W) alipopigana, haikuwa kuwashurutisha wasioamini kumfuata katika itikadi yake, bali ilikuwa kuleta uhuru kwa watu kuchagua dini waliyoipenda, kukomesha mateso kwa watu waliofuata dini waliyoipenda, na kulinda nyumba za ibada za dini zote. Kurani Tukufu yasema. ‘Ruhusa ya kupigana imetolewa kwa wale

ambao wamedhulumiwa. Na ikiwa Mungu Hangewaruhusu baadhi ya watu kuwafukuza wengine, nyumba zote za dini, ambamo jina la Mungu linakumbukwa sana zingeangamizwa' (22:40,41).

Tena Kurani Tukufu yasema, 'Piganeni katika njia ya Mungu na wale wanaopigana nanyi' na 'Piganeni nao ili kwamba kusiwe na kutesana kwa dini na kwa sababu hiyo dini itakuwa kwa Mungu tu' (yaani, kila mmoja atakuwa huru kufuata dini ambayo ataipenda kwa sababu ya Mungu) (2: 191 na 194): Aya hizi za Kurani Tukufu zathibitisha kwa wazi kuwa sababu ya Mtume Mtukufu (S.A.W) kupigana haikuwa kulazimisha watu kuikubali itikadi yake.

Mtume Mtukufu (S.A.W) na wafuasi wake Hawakuachiliwa na maadui zao wa Makka kuishi kwa amani katika madina ,Mateso yaliendelea na yakawa mabaya zaidi. Watu wa Makka mwishowe walikata shauri kuangamiza Islam na Waislam wote. Mapigano ya kwanza ya Mtume (S.A.W) yanajulikana kwa jina la mapigano ya Badr. na yalipiganwa karibu mwaka mmoja baada ya Mtume (S.A.W) kuhamia Madina. Hakukuwa na sababu yoyote kwa watu wa Makka kupigana vita na Mtume (S.A.W) na wafuasi wake. Kulikuwa na Waislam 313 na baadhi yao walikuwa vijana wadogo. Wote hao hawakuwa na silaha za kufaa hata kidogo. Maadui walikuwa elfu moja na walikuwa na silaha nzuri na nyingi. Kwa hivyo haiwezekani kuwa Waislam ndio waliotaka vita. Ni watu wa Makka waliotaka kupigana na Waislamu na kuwageuza kuacha dini yao. Hii tu ndiyo sababu ya mapigano yote yaliyopiganwa na Wamakka. Lakini ijapokuwa hesabu ya watu wa Makka ilikuwa kubwa sana. kila wakati walishindwa na Waislam.Tokeo moja la matata haya na mapigano hayo ni kuwa Mtume Mtukufu (S.A.W) aliweza kuonyesha utukufu wa tabia na utu wake na

pili dunia nzima iliona moyo wa mapenzi makuu na usiojipenda uliokuwa tayari kutumikia, ambao Mtume (S.A.W) alikuwa ameuamsha katika wafuasi wake.

**Vita vya Uhud.**

Hiki ndicho kisa cha mapigano ya Uhud, nacho kisa hiki chaonyesha jinsi wafuasi wa Mtume Mtukufu (S.A.W) walivyompenda, Ilipotimia miaka mitatu tangu Waislamu wahamie Madina, adui wapiganaji 3000 walitoka Makka kwenda kuihujumu Madina, Umbali wa maili mia mbili kutoka Makka. Maadui hao walikuwa na hakika sana kuwa watashinda hata wakajongea karibu sana na Madina katika mashambulio yao. Mtume Mtukufu (S.A.W) alitoka na watu 700 kuwapiga maadui. Mapigano hayo yalipiganwa huko Uhud, maili 8 kutoka Madina. Kikosi kimoja cha watu wa Mtume (S.A.W) kilikosea katika kufahamu amri zake, kwa hivyo, badala ya kushinda mapigano hayo kama ilivyokuwa yaelekea kuwa walikuwa wanashinda, kwa kosa hili walishindwa. Maadui waliwarejesha Waislam nyuma sana, Mtume (S.A.W) akaachwa peke yake nyuma katikati ya maadui waliomzunguka pande zote, lakini alisimama imara na kupiga ukelele kuwaita askari zake kuja kwake. Watu wake waligundua kosa lao halafu wakaanza kujaribu sana ajabu kwenda kumsaidia, lakini watu kumi na wanne tu baina yao ndiyo walifaulu kujipenyeza katika mistari ya maadui. Hapo Mtume Mtukufu (S.A.W) alipigwa jiwe kichwani, likamkata na akaanguka chini. Alifunikwa chini ya maiti za Waislamu walioangushwa wakijaribu kumsaidia. Ilifikiriwa kuwa Mtume Mtukufu (S.A.W) amekufa. Wafuasi wake waliposikia habari hii waliumizwa moyoni sana ajabu. Macho ya wengi wao yalijaa machozi. Askari mmoja wa Kiislamu aliyekuwa mpita njia huko.mjini aliuliza sababu ya huzuni hii. Alipoelezwa habari zilizoletwa na watu wengine kutoka kule kwenye uwanja wa vita juu ya kifo cha Mtume

(S.A.W) alisema kuwa kama ni kweli, wakati huu sasa ni wakati wa mapigano makali zaidi. “Tutamtafuta Mwongozi wetu mpaka kufa”. Baada ya kusema hivi alitoa upanga wake na kuwashambulia maadui, na yeye mwenyewe aliuawa mwishowe.Majeraha ya panga yasiyopungua themanini yalikuwa juu ya mwili wake ulipogunduliwa baadaye. Jina lake lilikuwa Anas-bin-Nazar (Furaha ya Mungu iwe juu yake).

Mwili wa Mtume (S.A.W) ulipatikana chini ya maiti za wafuasi wake. Hakuwa amekufa, bali hai! Habari hiyo ilienea na jeshi la Waislamu lilikusanyika pamoja tena na kupigana na kuwashinda maadui.

Askari mmoja Mwislamu alikuwa akimtafuta jamaa yake aliyepotea na akamwona amejeruhiwa sana karibu kufa. Mara tu mtu huyo aliyekuwa karibu kufa alipomwona mwenziwe, alimwuliza habari za Mtume (S.A.W) na akaambiwa kuwa ni salama. Uso wa mtu huyo aliyejeruhiwa vibaya ukang’aa kwa furaha alipokuwa akisema. ‘Sasa nakufa na furaha’. Majeruhi huyo halafu aliushika mkono wa jamaa Yake na kumwambia kupeleka habari hii kwa jamaa waliokuwa wa ukoo wake na wapenzi wake: ‘Muhammad (S.A.W) Mtume wa Mungu ni Amana katika mikono yetu, tuliyopewa kuweka na Mungu, ambayo itatulazimu tujibu kwa Mungu jinsi tulivyoitunza. Ni wajibu wenu kulinda amana hii tukufu. Muwe waangalifu kuona kwamba hamshindwi kutimiza wajibu wenu. Hivi ndivyo Waislamu walivyoonyesha uaminifu wao kwa Mtume Mtukufu (S.A.W).

Habari ilipofika Madina kuwa Mtume (S.A.W) ameuwawa. watu wa Madina walitoka mjini kwenda kwenye uwanja wa vita na nyoyo zilizojaa huzuni. Walikutana na jeshi la Waislam likirejea pamoja na Mtume (S.A.W) akiwa salama. Mwanamke mmoja

alijongea mbele na kumwuliza askari mmoja ‘Yu hali gani Mtume? Askari huyo alijua kuwa ni salama, hakujisumbua kumjibu swali, bali alisema, ‘Baba yako ameuwawa Bibi’. Yu hali gani Mtume wa Mungu? Mwanamke aliuliza kwa haraka. “Sikuuliza habari za kifo cha baba yangu”! Tena askari hakuwazia kumwondolea mashaka mwanamke huyo kwa kumweleza habari ya Mtume (S.A.W) bali alijibu “ Wale ndugu zako wawili wamekufa, dada mpenzi”. Mwanamke huyo hakuweza kusubiri tena na alisema kwa hamaki: “Sikuulizi unieleze yaliyotendeka kwa ndugu zangu” Waweza au huwezi kunieleza jinsi hali ya Mtume wa Mungu (S.A.W) ilivyo? ‘Mtume Mtukufu (S.A.W) yu salama kabisa’askari alijibu. Mungu Asifiwe! mwanamke huyo alisema: Ikiwa Mtume wa Mungu (S.A.W) yu hai basi dunia yetu ni hai, na sijali nani mwingine anakufa’. Vipi mapenzi kama hayo ya kweli juu ya Mtume (S.A.W) kuwamo ndani ya nyoyo za wafuasi wake, ikiwa yeye mwenyewe hakuonyesha mfano mzuri na kamili na hadhari kubwa kwa furaha ya wanadamu?

## SURA YA TISA

### Kisa cha Hunain na nguvu za Utume

Siku moja jeshi la Waislamu lilikuwa likipita katika njia ya nafasi iliyokuwa kati ya milima na maadui walikuwa wamejificha pande zote mbili za njia hiyo. Waislamu hawakujua mpango wa maadui, ambao walipowaona walianza kuwapiga mishale. Jambo hili liliwashtua farasi na ngamia wa Waislamu, na wapandaji walishindwa kuwaongoza kama walivyotaka. Mtume Muhammad (S.A.W) akiwa na wafuasi kumi na sita peke yao waliachwa katika jeshi la maadui lenye askari elfu nne. Vikosi vingine vya Waislamu vilitawanyika pande zote. Mtume Mtukufu (S.A.W), pasipo woga, alimwongoza farasi wake kuwaelekea maadui. Kuona hivi, wafuasi wale wachache aliokuwa nao kwanza hawakujua watafanya nini; lakini papo hapo mmoja wao upesi alishuka kwenye farasi wake na kumshika farasi wa Mtume Mtukufu (S.A.W) na kusema: ‘Maadui wanakuja mbele, jeshi la Waislamu halijajitayarisha, na usalama wa Waislamu unategemea usalama wako, tafadhali rudi nyuma, ili Waislamu waweze kukusanyika na kuwa pamoja.”Usimzuie farasi wangu” Mtume (S.A.W) alisema. Halafu akasema kwa sauti ya juu ‘Mimi ni Mtume wa Mungu. mimi si msemaji wa uwongo. mwache anidhuru awezaye.’ Akisema maneno haya, aliendelea mbele kwa kuwahujumu maadui. Hakuna mkono wa mwanadamu ulioweza kumdhuru. Hapo Mtume (S.A.W) alimwamrisha mmoja katika wafuasi wake kuwaita kwa sauti ya juu Waislamu waliokuwa wamekimbia akisema: ‘Enyi watu wa Madina. Mtume wa Mungu anawaiteni. Mmoja wa wafuasi wa Mtume; (S.A.W) baadaye alisema: ‘Farasi wetu na ngamia wetu walikuwa wametishika vibaya sana na walikuwa wamekimbia kutoka kwenye vita; jitihada zetu za kuwarejesha zilishindwa.

Tulipousikia mwito huu ikawa kana kwamba ni sauti ya Mungu ikisema nasi. Na nilihangaika. Maneno 'Mtume wa Mungu anakuiteni' yaliendelea kusikika katika masikio yangu. Nilipomwona ngamia wangu bado ananielekeza mbali kutoka kwenye uwanja wa vita. nilichukua upanga wangu na kumwua. Halafu nikakimbia mbio mbio kama mtu mwenye wazimu kuelekea kule sauti ilikotokea.' Bwana huyu alisema "Waislamu wote walikuwa na hali hiyohiyo. Mtu yeyote aliyeweza kumgeuza farasi wake au ngamia alirudi. na wale ambao hawakuweza kufanya hivyo. walishuka na kumkimbilia Bwana wao. Baada ya dakika chache askari wale walimzunguka Mtume (S.A.W) baada ya kusikia mwito wake kama vile maiti watakavyoinuka kwa sauti ya baragumu la malaika Israfili."

Mtume mtukufu (S.A.W) kila wakati aliwaambia wafuasi wake kwamba wasiwe wa kwanza kuhujumu. Lakini kila mara wapigane kwa kujihami nafsi zao. Pia alisema katika vita wasiwauwe wanawake, wala watoto wala viongozi wa dini, wala wazee, wala wale walioweka panga zao chini. Miti isikatwe, wala majumba yasiharibiwe, wala wasinyang'anye katika miji wala mabonde. Kila aliposikia kuwa amri zake hizo zimevunjwa alikasirika sana.

Mungu Alipomruhusu Mtume (S.A.W) kuiteka Makka watu wa Makka waliogopa sana adhabu ambayo wataipata kutoka kwake, Lakini alipoingia Makka aliwakusanya watu wa Makka pamoja na kuwaambia. 'Enyi watu, leo nakusameheni makosa yote mliyonifanyia, hamtaadhibiwa.

Vita alivyopigana Mtume (S.A.W) vyaonyesha umashuhuri wa utu wake, mapenzi yake kwa amani, huruma na kusamehe kwake, kwa sababu yeye peke yake ndiye mwenye huruma kabisa ambaye ana uwezo wa kuonyesha huruma na

anaionyesha. Yeye peke yake ndiye anayestahili kuitwa mkarimu ambaye anao utajiri na anaugawa. Mungu Mwenye uwezo wote Alimruhusu Mtume (S.A.W) kuwashinda maadui zake na aliwasamehe wote. Yeye aliyafanya ambayo aliwaamrisha wengine kuyafanya. Aliteseka kwa ajili ya Mungu. Alifariki akiwa na umri wa miaka sitini na mitatu, baada ya kutumia maisha yake yote kwa kuhubiri juu ya Mungu Ambaye ni Mmoja tu, na msaada wowote unaopatikana leo duniani kwa mafunzo haya yote ni matokeo ya kazi ya Mtume Mtukufu (S.A.W) na kazi ya wale waliomfuata.

**Hotuba ya mwisho ya Mtume (S.A.W)**

Mtume (S.A.W) alikwenda hija yake ya mwisho katika mwaka wa 10 A.H. (yaani mwaka wa kumi tangu kuhama Makka). Wakati huo nchi yote ilikuwa imekubali Islam. Kadiri ya jumla ya watu 124,000 kutoka pande zote za Bara Arabu walikusanyika pamoja kwa tukio hili.

Tamasha ya ajabu hii! Mahali pale. ambapo Mtume (S.A.W) pamoja na kutoaminiwa aliteswa na ikalazimu kuhama, ndipo mahali sasa ambapo kulikuwa na mkutano mkubwa sana wa wafuasi waaminifu. Mtume Mtukufu (S.A.W) alijua sasa kwamba kazi aliyopewa kufanya duniani imetimizwa. Jitihada zake zilipata mafanikio ambavyo mtu mwingine hajapata kufaulu kufanikiwa hivyo. Kwa hivyo, alikaribia kuacha kuendelea kuishi maisha ya dunia hii.

Hotuba aliyotoa Mtume (S.A.W) kwa wakati huu haikuwa ya kawaida, na huu ndiyo wakati uliofaa zaidi kwa hotuba hiyo. Hapa palikuwa mahali ambapo kulikuwa mapigano na mauaji. Hilo kundi kubwa sana la watu lilikuwa limekusanyika ili watu wamshukuru Mungu na kuusifia Ukuu Wake kwa wakati huo

wakisahau na kutupilia mbali mambo yote ya kidunia. Hapa watu wote walikuwa sawa hakukuwa na dalili yoyote ya tofauti kati ya mfalme na masikini. Wale walikutana kama ndugu kumwonyesha heshima Bwana wao Aliye juu mbinguni. Mahali hapo, kwa hivyo, Waislamu wote yawalazimu kujaribu kwenda kupaona kwa uchache mara moja katika maisha yao.

**Mji wa Makka jinsi unavyoonekana katika siku za Haji**

Mtume (S.A.W) alikaa juu ya ngamia na watu walimzunguka pande zote katika bonde la Minaa. Maneno yake yalienezwa na watangazaji wengine ili yapate kusikiwa na watu wote waliokuwako. Hii ndiyo hotuba ya Mtume Mtukufu (S.A.W):-

"Sikilizeni maneno yangu, kwa kuwa sijui kama tutapata kuonana tena mahali hapa. Mwajua hii ni siku gani? Ni siku ya Yaum-un-Nahr, iliyo siku tukufu. Mwajua mwezi huu ni mwezi gani? Huu ndiyo mwezi mtukufu. Mwajua mahali hapa ni mahali gani? Huu ndiyo mji mtakatifu. Kwa hivyo nawaambia kwamba maisha yenu. mali yenu na heshima zenu lazima vifikiriwe vitakatifu na kila mmoja kwa mwenziye kama siku hii tukufu. Katika mwezi huu mtukufu. katika mji huu mtukufu. Watu waliohudhuria hapa wawapelekee habari hii wale ambao hawakufika.

Mtaonana na Bwana wenu, atakayewahukumuni kwa yote mliyoyatenda.

Siku ya leo pesa zile ambazo zadaiwa kama riba ziachiliwe. Siku ya leo kulipiza kisasi kwa mauaji yaliyofanywa katika siku za kabla ya Islam kumekomeshwa.

Kumbukeni, Enyi watu wangu, mna haki kadhaa juu ya wake zenu, na vile vile wake zenu wana haki juu yenu. Wake ni amana za Mungu mikononi mwenu. Kwa hivyo yawalazimu kuwatunza kwa huruma na upole. Na juu ya watumwa wenu, angalieni sana kwamba mnawapa ambacho nyinyi wenyewe mwakila, na mwavike kama nyinyi wenyewe mnavyovaa.

Enyi watu! sikilizeni ninayosema na myakumbuke. Lazima mfahamu kwamba! kila Mwislamu ni ndugu wa Mwislamu mwingine yeyote. Ninyi nyote ni sawa na haki zenu ni sawa na pia wajibu wenu ni sawa. Ninyi nyote ni ndugu.

Haifai kwa yeyote baina yenu kuchukua kitu cho chote kutoka kwa ndugu yake kama ndugu hana moyo wa kupenda kugawa kitu hicho pasipo manung'uniko.

Msiwadhulumu watumishi wenu, msiwanyang'anye haki zao.

Mwisho wa hotuba yake Mtume (S.A.W) aliinua juu mikono yake na kuuliza nimetimiza ujumhe ambao Mungu Aliniamuru kuwaletea? 'Umetimiza,' kundi hilo kubwa lilijibu. Halafu aliwaomba wale williohudhuria kuwapelekea habari hizo wale ambao hawakuwa hapo.

## SURA YA KUMI

### Tabia ya Mtume (S.A.W).

Kurani Tukufu yasema hivi juu ya Mtume (S.A.W): “Na bila shaka una tabia njema tukufu” (68:5). “Bila shaka mnao mfano mwema katika Mtume (S.A.W) wa Mwenyezi Mungu - kwa mwenye kumwogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na kumtaja Mwenyezi Mungu sana” (33:22).

‘Tabia zake ndiyo Kurani’, ndiyo maneno ambayo Bi Aisha (furaha ya Mungu iwe Juu yake), mke wa Mtume (S.A.W), alitamka, aliyejua maisha ya ndani kabisa ya Mtume (S.A.W), katika kueleza tabia na matendo ya Mtume (S.A.W). Kawaida ya maisha yake ya kila siku illkuwa mfano bora wa mafundisho ya Kurani. Kwahiyo Mwislam ana viongozi wawili - Kurani Tukufu yamweleza jinsi inavyofaa aishi; namaisha ya Mtume (S.A.W) ni mfano bora wa kuishi.

Tabia ya Mtume Mtukufu (S.A.W) ilikuwa thabiti na nyepesi kuelea. Mambo haya yalikuwa sehemu ya utu wake. Aliweza kutenda mambo yote kwa mikono yake mwenyewe alisaidia katika kujenga msikiti Madina. Na alibeba mawe mpaka kule yalikotakiwa kwa kujenga ukuta. Alipotaka kumpa masikini pesa. Kwa mikono yake mwenyewe alizitia hizo pesa katika mikono ya masikini. Aliwasaidia wake zake katika kazi zao za nyumbani. Aliwakamua mbuzi wake na kuzipiga viraka nguo zake ziliporaruka na pia viatu vyake. hakuna kazi aliyoidharau kuwa kazi ya chini kwake.

Alikwenda dukani na kujinunulia vifaa na kwa jamaa yake, hata aliwanunulia na marafiki pia mahitaji yao ya nyumbani. Alifanya mambo haya yote ingawa alikuwa mtume na Mfalme,

akionyesha, kwa mfano wake mwenyewe kwamba si cheo cha mtu kinachomfanya mtukufu, ila ni wema wake na matendo yake mema kwa wengine. Kibarua anayetunza barabara, ama kibarua mwenye kupasua kuni na kuteka maji, astahili heshima kubwa katika udugu wa Islam kama mfanya biashara mkubwa ama mtu mashuhuri katika utawala wa nchi.

Mtume (S.A.W) alijifanya mtu wa kawaida mwenye njia za kujirahisishia sana (amani na baraka ya Mungu viwe juu yake) katika mambo yake yote hata kama ni mtumwa aliyemwalika, yeye alikubali tu. Alikula chakula chake pamoja na watu wa vyeo na madaraka mbalimbali na ya kila aina, hata na watumwa.

Alipokuwa katika kundi la watu pengine alinyamaa kwa muda mrefu. Kama kulikuwa na jambo la kusema juu yake, alisema, lakini hakupenda kusema kwa ajili ya pendo la kutaka kusema. Alipotoka nje watu walitembea mbele yake na wengine nyuma yake. Alipoketi pamoja na watu hakukuwa na jambo la kumtofautisha na hao watu wengine. Hakusema ikiwa Watu wengine walikuwa wakitoa habari zao, lakini alicheka pamoja na watu wakati wa kicheko ulipotokea. Alisema polepole sana hatamaneno yake yaliweza kuhesabiwa alipoyatamka.

Tabia ya Mtume (S.A.W) ya kuishi pia ilikuwa ni ya Kawaida katika kila alilotenda. Alipenda chakula ambacho Hakikuchanganyika aina nyingi za vyakula, na alikula chakula kile alichopewa ale, kama alivyokuwa akifanya alipokuwa mtoto.Kama chakula hakikumpendeza alikichukua na kukiweka kando wala asinung'unike na kuteta na wapikaji wa hicho chakula. Chakula cha kitajiri kilipoandaliwa kwake, alikila lakini kwa kawaida alikula aina moja tu ya chakula katika wakati mmoja. Alipenda sana  asali.Hakupenda vitu vyenye harufu kali sana.

Mtume Mtukufu (S.A.W) alipenda usafi, na aliweka mwili wake katika hali ya usafi wakati wote. Alipiga mswaki meno yake mara kadhaa kila siku.Pia alitumia mafuta yenye kunukia vizuri. Alinawa mikono yake kabla na baada ya kula.

Katika mavazi yake Mtume (S.A.W) alivaa kikawaida. Hakuona ubaya katika kuvaa nguo zilizopigwa viraka, lakini pia hakuzichukia zile za kitajiri. Hakupenda wanaume kuvaa nguo za hariri, alitaka waonekane wanaume kweli. Alikuwa mwangalifu sana kuona kwamba alivaa nguo zake njia ile ya kanuni ya mtindo.

Nyumba ya Mtume (S.A.W) ilikuwa ya vyumba vidogo vidogo, na ilijengwa kwa matofali ya udongo. Alikuwa na kitanda na mkebe wa maji katika chumba chake, Hivi ndivyo alivyoishi hata baada ya kuishinda Khaibar. Siku nyingi ziliweza kupita pasipo moto kuwashwa katika nyumba yake kwa ajili ya kupika. Jamaa zake wote walikuwa na tende na maji peke yake kwa chakula chao. Aliifikiria dunia hii kama mahali ambapo mtu anaishi kwa muda mfupi tu.

'Hali yangu mimi' alisema siku moja, 'ni kaima ile ya msafiri ambaye adhuhuri anasimama chini ya kivuli cha mti kupumzika kwa muda mdogo, kabla ya kuendelea na safari yake zaidi'. Hakuna utajiri ama starehe.

Mtume (S.A.W) alikuwa na pendo kubwa kwa rafiki zake, na mkarimu kwa adui zake. Alimwendea kila mtu akiwa na tabasamu usoni mwake, na aliposalimiana kwa mikono na watu, hakupata kuwa wa kwanza kuacha mkono wa mwenziye. Hakusema mengi juu ya nafsi yake mwenyewe. Alipenda kuwabeba watoto wa rafiki zake katika mikono yake kama baba. Hakupenda mazungumzo yasiyo na fikra ndani yake

juu ya watu wengine, alipenda hasa kufikiri uzuri juu ya watu wote. Alipenda kuwa wa kwanza kuwaamkia rafiki zake, mara nyingine akiwaita kwa majina yao ya kawaida kuwaonyesha pendo alilokuwa nalo juu yao. Ikiwa mtu alipata kumsaidia, siku zote baada ya hapo alithamini urafiki kati yake na mtu huyo. Alipohubiri , alionyesha jinsi ya kuepuka katika kutenda jambo baya, pasipo kumfanya mtu yeyote kufikiri kwamba alikuwa anaeleza habari zinazomhusu yeye. Alichukia udanganyifu na uwongo.

Ukarimu wa Mtume (S.A.W) kwa adui zake ni wa pekee katika historia ya ulimwengu. Watu wa Makka ambao walimtesa sana ajabu yeye na rafiki zake walipata msamaha wake, hata pasipo kuombwa. Jinsi mshindi anayefuatana na mambo ya kidunia angetenda yaweza kuonekana wazi. Mateso yaliyoendelea hata miaka kumi na mitatu yalisamehewa na kusahauliwa. Mahabusu waliokuwa mateka wa vita waliachwa huru pengine jumla ya watu elfu sita walifunguliwa kwa wakati mmoja - Wayahudi, Wakristo na watu wanoabudu masanamu walitendewa hivyo. Hakutenga huruma yake kuwa kwa wafuasi wake peke yao. Haki ilikuwa sawa kwa wote, rafiki na kwa maadui pia. Uamuzi wake wa ugomvi ulikubaliwa na watu wote.

Simulizi kutoka kwa Anas (furaha ya Mungu iwe juu yake) anasema kwamba katika muda wa miaka kumi ambapo alimfanyia Mtume (S.A.W) kazi, hakulaumiwa naye hata mara moja. Mtume (S.A.W) hakupata kulaumu watumishi wake kwa makosa yao, na hakumweka mtu yeyote katika utumwa kila alipopata mtumwa, alimwacha huru. Katika maisha yake yote hakupata kumpiga mtumishi ama mwanamke.

Mtume (S.A.W) hakupata kukataa kumpa masikini mwombaji. Aligawa hata kama kufanya hivi kulimweka katika hali mbaya.

Aliwalisha waliokuwa na njaa, pengine yeye mwenyewe akiishi pasipo chakula. Hakujiwekea pesa mwenyewe. Alipolala kitandani akifariki dunia aliitisha pesa zote zilizokuwa nyumbani kwake kuletwa, na kuzigawia masikini. Moyo wake ulijaa huruma kwa wanyama wote, na moyo wake wenye huruma ulimsikitikia mtu yeyote aliyekuwa katika mashaka. Aliwatembelea wagonjwa na kuwafariji, na hakupata kukataa kwenda mazishini.

Mtume Mtukufu (S.A.W) hakupata kusikiwa akitumia maneno mabaya kama ya matusi. Hakusema kwa ukali. Aliwatembelea wagonjwa na kuwafariji, na siku zote alikuwa mwangalifu kwa kuwatendea wema wageni kwa kadri alivyoweza, na alitumia nao kila alichokuwa nacho. Alikuwa mwenye adabu kwa wazee na vijana. Kila mara bibi aliyemlea mama yake alipofika, na dada yake alipoingia alipokuwa, Mtume (S.A.W) alisimama, na aliwatandazia chini shuka lake mwenyewe ili wakalie. Alikuwa na heshima kadiri hiyo kwa binti yake mwenyewe, 'Muwape heshima watoto wenu' alizoea kusema, na pia, 'Pepo iko miguuni mwa mama wazazi'

Katika vitabu juu ya maisha ya Mtume (SAW) ambavyo viliandikwa na watu ambao wengine wao walikuwa marafiki zake, na wengine hawakusadiki mafunzo yake, waandishi hawa wote wasifia ushujaa wake katika nyakati za taabu kubwa ajabu na hatari nyingi, na nyingi ni hadithi za kuonyesha ushujaa huu.

Siku moja mtu ambaye Mtume Mtukufu (S.A.W) hakuwa anamfahamu hata kidogo alimjia na kumwambia kuwa Abu Jahl alikuwa menunua ngamia kutoka kwake lakini alikataa kuwalipia ngamia hao mtu huyo alimwomba Mtume Mtukufu (S.A.W) kuandamana naye kwenda kwa Abu Jahl kupata hizo

pesa. Abu Jahl ndiye aliyekuwa adui, mkali zaidi katika maadui wa Mtume Mtukufu (S.A.W) lakini hii haikumzuia Mtume (S.A.W) kuliitikia ombi la mtu yule. Mtume (S.A.W) na yule masikini walikwenda wote kwa Abu Jahl na Mtume (S.A.W) akamwomba kulipa zile pesa. Abu Jahl alishangaa sana kumwona Mtume (S.A.W) akimwendea kwa jambo hili hata akazilipa pesa mara moja.

Wakati mwingine akiwa safarini, Mtume (S.A.W) alikaa peke yake akipumzika katika kivuli cha mti. Mmoja wa maadui zake alipata kumkuta hapo, halafu akachomoa upanga wake alani akasema; “Ni nani anayeweza kukuokoa mikononi mwangu? Mtume (S.A.W) hakuogopa hata kidogo, na alitamka neno moja tu “Allah” Mara upanga wa mtu huyo ulianguka chini kutoka katika mikono yake. Hapo Mtume (S.A.W) akauchukua na kusema: “Ni nani anayeweza kukuokoa mikononi mwangu sasa? “Hakuna” alijibu mtu huyo” “Basi jifunze kutoka kwangu jinsi ya kuwahurumia watu”, alisema Mtume s.a.w. na kumruhusu mtu huyo kwenda zake. Mara mtu huyo akamwamini Mtume (S.A.W).

**Mafundisho ya Mtume s.a.w.**

Mtume (S.A.W) alifundisha kwamba kuna Mungu Mmoja peke Yake, na kwamba viumbe vyote, Malaika na Binadamu ni viumbe vya Mungu.

Alifundisha kwamba Mitume wote walikuwa watumishi wa Mungu na kwamba hakuna mmoja wao aliyekuwa na uwezo sawa na wa Mungu. Kwa hivyo binadamu wote yawapasa kumwomba Mungu Aliye Mmoja, na wamwabudu Yeye peke Yake, na kumtegema Yeye tu.

Alifundisha kwamba Mungu Alikuwa Ametuma Mitume Wake kwa mataifa yote katika nyakati zilizopita.

Alifundisha kwamba iliwapasa watu kuishi kwa amani baina yao, hata kama ni wa dini mbalimbali, na yeye mwenyewe siku moja aliwaruhusu Wakristo kukutana kwa ibada yao kwa Mungu katika msikiti wake.

Alifundisha kwamba roho ya mtu iliumbwa na Mungu kuishi milele na kwamba hata watu waovu baada ya kuadhibiwa na kusafishwa uovu wote waliokuwa nao, wataweza kuendelea pamoja na wengine katika huruma ya Mungu isiyo na mipaka.

**AMANI NA BARAKA ZA MUNGU ZIWE JUU YA MTUME MUHAMMAD S.A.W.**

.